Ukweli Hauna Kutu

# Pambazuko

Toleo Namba 006 Jumatatu Agosti 15 -21, 2022

**Uk. 3 - Rais asiwe mama wa barabara, madaraja**



# Mafuta: Zigo zito kwa Rais Samia

● *Wachumi washauri ruzuku kwa dizeli tu*


**Uchaguzi: Tuige Kenya au waige Tanzania?**

**Uk. 6**

**Tupunguze umaskini kuondoa ugaidi**

**Uk. 8**

**JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure**




## Jisajili kupata Pambazuko bure

Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** na kutuma neno **"HABARI"** ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

Pia unaweza kujisajili kwa kutumia Email hii: **pambazuko1@protonmail.com** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **"HABARI"** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

# Rais Samia asiwe mama wa barabara, madaraja

**Na Plato Hekimachius**

WIKI iliyomalizika jana, Tanzania ilikuwa ikifuatilia kwa karibu ziara ya Rais Samia Suluhu Hassan katika mikoa ya Mbeya, Njombe na Iringa.

Ukiitazama ziara ya Rais Samia huko maeneo ya nyanda za juu, utagundua kwamba kuna kitu kimoja kinajitokeza kila mahali. Rais anawaeleza wananchi namna serikali inavyowajali, huku nao wananchi wanamweleza kuhusu changamoto zao.

Rais anaeleza kuwa serikali inawathamini, inashughulikia kero zao na ina upendo wa kweli kwao. Wananchi nao wakiwa wamejitokeza kwa wingi kumsikiliza - huku wakiwa wanapunga bendera za chama cha rais; wachache wanapewa kipaza sauti na kuambiwa waseme nini na rais anaandaa wa kujibu. Baada ya hapo, safari ya Rais Samia na msafara wake inaendelea kuelekea kituo kingine.

Ukitazama kwa umakini unagundua kuwa katika ziara za wakubwa wa nchi, mara nyingi nyuma ya pazia wasaidizi wa rais wako bize 'kununua upendo' kwa ajili ya rais. Na pengine baadhi ya 'wapinzani' wanaitwa kukutana na rais kwa siri. Wanamuahidi na yeye anawaahidi.

Wanapogundua hili, baadaye makada wa chama cha rais wanalia mbele yake kwa kusahaulika. Wanaahidiwa kukumbukwa. Wateule na wabunge wanapanda majukwaani wanamweleza rais alivyo mzuri na alivyomwaga fedha mpaka kero za eneo zikahamia Zimbabwe! Ziara inafika mwisho, kero zinabaki na pengine zinaongezeka, rais ametimiza wajibu wake.

Watangulizi wa Rais Samia nao walifanya ziara, waliweka mawe ya msingi, walizindua miradi, walijenga shule, madaraja, hospitali, machinjio, mashamba na mbuga za wanyama. Wako wapi? Wamekufa, wengine



*Rais Samia Suluhu Hassan,*

wapo, na hatuwazungumzii tena au tukiwazungumzia tunawakejeli kwa njia ya kumsifia huyu aliyepo. Naye ajue akitoka gurudumu la mambo haya litaendelea kuzunguka. Ni kawaida. Kwa nini?

Watangulizi kadhaa wa Rais Samia leo wamesahaulika kwa kuwa walitumia fedha na muda kufanya vitu vinavyoisha thamani na ambavyo hata shetani akipewa nchi atafanya tu. Hawakuwekeza katika mioyo wala thamani ya utu, heshima na haki za msingi za watu. Waliwekeza katika matumbo ya baadhi ya watu na mifuko yao.

Binadamu walivyo - ni wepesi kusahau, ukitenda mema, utadumu mioyoni mwao, ukiwaonea au kuruga utaratibu wa maisha yao, wanakusahau.

Rais Samia afanye nini kuvunja utamaduni huu? Laiti angeshauriwa, akasikia na kukubali kuwafanyia kitu ambacho Watanzania hawakufanyiwa na marais waliopita ili wamkumbuke daima dumu ni; KATIBA MPYA.

Akifanya kuwapa Katiba Mpya, atakumbukwa kama Mama wa Demokrasia na Uhuru wa pili. Picha yake itakaa sambamba na picha ya Julius Kambarage Nyerere, ambaye ni Baba wa Uhuru wa kwanza na Baba wa Taifa hili.

Rais Samia achague kutokuwa Mama wa Madaraja na Barabara. Mafuriko yakija tutamsahau.

# Uchaguzi: Tuige Kenya au waige Tanzania?

**Na Dkt. Bullet Ruhinda**

HABARI kubwa ya wiki nzima iliyopita ni utulivu ulioonekana kabla, wakati na baada ya kupigwa kwa kura katika uchaguzi mkuu wa Kenya.

Uchaguzi mkuu wa nchi hiyo ulifanyika Agosti 9 mwaka huu.

Maongezi ya mitandaoni na vijiweni ni kwamba Tanzania tuna mengi ya kujifunza kutoka katika uchaguzi huo, hasa kuhusu uwazi na utaratibu wa kirazini uliotumika katika usimamizi wake.



Lakini, hivi majuzi kaibuka kiongozi mmoja mkubwa, na kasema kwamba Kenya wana mengi ya kujifunza kutoka kwetu Tanzania. Wasikilizaji wake wakashangilia.

Kiongozi akanogewa na kuwauliza kama kuna mtu aliwahi hata kupigwa konzi wakati wa uchaguzi wa Tanzania.

Nilitegemea wasikilizaji wa mkubwa yule, na hasa wale wenye uwezo wa kufanya ulinganisho wa kirazini, wayashangae maneno kwamba, Kenya wana jambo la kujifunza kutoka uchaguzi wa Tanzania.

Je, ni lazima kwamba uchambuzi wa kirazini unaofanywa na kiongozi ndio lazima uwe ni uchambuzi wa kirazini kwa raia wote? Hebu tutafakari pamoja kidogo.

Nataka tujiulize: Je, ni kweli kwamba, uamuzi wa kirazini unaofanywa na mtu mmoja ni lazima uonekane uamuzi wa kirazini kwa watu wote baki?

Hebu tuanze na mfano rahisi wa kushangaa. Je, kwa nini tunashangaa? Je, mtu anaweza kujizuia kushangaa? Je, tunashangaa katika mambo gani? Je, kila kinachokushangaza kitashangaza wengine?

Kwa mfano, nilipofika Dar es Salaam mara ya kwanza baada ya kutoka kijijini kwetu, nilikozaliwa na kukulia, niliyashangaa maghorofa marefu maana kwetu hayapo.

Lakini, je, ni kweli maghorofa haya yanapaswa kumshangaza kila mtu? Hapana. Ubongo wa mwanadamu ndio unaomua kipi cha kushangaza na kipi hakishangazi.

Vivyo hivyo, ni ubongo huo unaotwambia ni kitu kipi cha maana na kipi siyo chenye maana, kipi kinazingatia kanuni za urazini na kipi kinazikiuka.

Hivyo, ukimrusu mtu akuchagulie kitu kipi chenye ubora ujue una tatizo. Tatizo ni kubwa zaidi kwa nchi kama watu wengi bado wanategemea mtu mmoja, awaamue kitu gani ni bora.

Wakenya wamevuka kizingiti hiki kwa sababu ya kiwango cha elimu miongoni mwa wapiga kura.

Kwa mujibu wa takwimu za shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia elimu (Unesco), asilimia ya wapiga kura wenye kiwango cha elimu ya angalu kidato cha nne miongoni mwa Wakenya ni zaidi ya 25 wakati nchini Tanzania ni chini ya 10.

Tofauti hiyo ina maana kubwa katika namna wapiga kura wanavyofikiri, kuhukumu na kutenda.

Kama hivyo ndivyo, mpango mkakati wa Wizara ya Elimu ya Tanzania unasemaje kuhusu asilimia ya wapiga kura wanaopaswa kuwa na kiwango cha elimu angalu ya kidato cha nne ifikapo mwaka 2050? Tafakari.

# FBI hawataki niwe rais – Trump



IDARA ya Ujasusi ya Marekani (FBI) imetupiwa lawana na aliyewahi kuwa rais wa 45 wa nchi hiyo – kwa awamu moja, Donald Trump, kwamba inapanga njama chafu ili asiongoze tena.

Jumanne iliyopita, Trump (76) alilalama kuwa idara hiyo, tangu aondolewe madarakani mwaka 2021, imekuwa ikifuatilia maisha na mienendo ya biashara zake kwa nia aliyoitaja kuwa "isiyofaa" na kumchunguza kila mara.

Kiongozi huyo aliyeingia madarakani mwaka 2017, alidai nyumba yake ya kifahari iliyoko Mar-a Lago, Florida, ilivamiwa na idara hiyo na kuondoka na vifaa ambavyo hakuvitaja.

Tayari uongozi wa FBI ulikiri 'kuvamia' nyumba hiyo na kufanya upekuzi wa nyaraka muhimu ambazo hakupaswa kuwa nazo nyumbani kwani zina siri kuu za nchi. Makasha 11 ya nyaraka hizo yalichukuliwa nyumbani kwa Trump.

Katika uchaguzi wa 2020, Trump alishindwa na mpinzani wake - rais wa sasa, Joe Biden, ingawa mpaka leo hajamtambua kuwa ni kiongozi wake.

***Marekani (Mashirika)***

# Maisha ya mwandishi hatarini

AFYA ya mwandishi maarufu wa vitabu, Salman Rushdie bado mbaya baada ya kugundulika kwamba anahitaji kufanyiwa upasuaji ili kuokoa maisha yake.

Rushdie alishambuliwa kwa kisu Ijumaa iliyopita Jijini New York, Marekani wakati akijiandaa kutoa mhadhara katika Taasisi ya Chautauqua kuzungumzia - "namna waandishi wanaokimbia nchi zao wanavyokuwa salama wakiwa Marekani."

Taarifa kutoka kwa mmoja wa wanasheria wake ameviambia vyombo vya habari kwamba kisu kilichotumika kumshambulia Rushdie kilitoboa jicho na kuchana ini.

Mwaka 1998, Rushdie aliingia matatani na Iran baada ya kiongozi wa nchi hiyo, Ayatollah Khomein kumtangazia kifo (Fatwa) kwa kuandika kitabu maarufu cha Satanic Verses (Aya za Shetani). Tangu wakati huo amekuwa akiishi kwa kujifichaficha, ingawa mwaka 2016 alianza kuonekana hadharani.

***Marekani (NYT)***

# Rais Ramaphosa 'apumua'

HOFU ya Rais wa Afrika Kusini kushitakiwa bungeni – kwa lengo la kumuondoa madarakani, imepungua baada ya wabunge wengi wa chama chake, ANC kutoonyesha nia ya kuendelea na mchakato huo.

Kulikuwepo wasiwasi mkubwa ulioshadidiwa na chama cha upinzani cha EFF na baadhi ya wanaharakati kutaka kumuondoa Rais Cyril Ramaphosa madarakani kwa madai ya kukiuka kiapo chake cha urais.

Inadaiwa kuwa Rais Ramaphosa aliibiwa kiasi kikubwa cha fedha kutoka katika shamba lake la mifugo la Phala-Phala, ambapo wengi wanahoji iweje kiongozi huyo awe na kiasi hicho cha fedha taslimu?

***Afrika Kusini (Daily Marverick)***

# Matokeo ya uchaguzi yashangaza

**Na Waandishi Wetu**

MATOKEO ya uchaguzi mkuu wa Kenya uliofanyika Jumanne iliyopita – Agosti 9, yanaendelea kushangaza wengi baada ya kuwepo kwa taarifa kwamba magavana wengi na wagombea wengine waliokuwa wakipewa nafasi ya kushinda, kuangushwa vibaya.

Wengi waliopoteza nafasi zao ni wale waliokuwa wakiunga mkono na kugombea kupitia muungano wa vyama ukiongozwa na Raila Odinga, ambaye pia alikuwa mgombea urais kupitia umoja huo.

Raila, alikuwa akipewa nafasi kubwa ya kushinda kiti cha urais, lakini matokeo yaliyokusanywa, yanaonyesha anapata upinzani mkubwa kutoka kwa Naibu wa Rais wa Kenya, William Ruto ambaye anagombea kupitia muungano wa vyama wa Kenya Kwanza.

Pamoja na kwamba hadi gazeti hili linaingia mtamboni, hakuna aliyetangazwa rasmi kuwa mshindi wa kiti cha urais, lakini ni dhahiri kuwa anayeweza kuibuka mshindi ni mmoja kati ya Raila na Ruto. Hawa wanaendelea kuchuana vikali kwa kuzidiana kura chache kila zinapoendelea kuhesabiwa.

Pamoja kwamba hakuna taarifa rasmi kutoka Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka ya Kenya (IEBC) kuonyesha wagombea wangapi na kwa nafasi gani ndiyo waliotawala ushindi, lakini kuna kila dalili kwamba chama cha Ruto kinaelezwa kunyakua viti vingi vya ubunge, ugavana, nafasi za wanawake na useneta.

Tayari, Gavana wa Laikipia, Ndiritu Muriithi (pichani) ambaye alikuwa mwenyekiti wa bodi ya kampeni ya Azimio la Umoja One Kenya, ni kati ya wanasiasa ambao walisombwa na mafuriko ya chama cha Ruto (UDA) katika eneo la Mlima Kenya.

Matokeo ya IEBC jana yalionyesha




kuwa Muriithi alipata kura 48,812 pekee huku Joshua Irungu wa UDA ambaye alikuwa gavana wa kwanza, akipata kura 113,380.

Katika uchaguzi wa 2017, Muriithi alimbwaga Irungu wakati huo akiwa mgombea huru licha ya chama cha Jubilee (kilichoungana na Raila katika uchaguzi huu) kutwaa viti vingi eneo hilo.

Kwa muhula mmoja aliokuwa kwenye uongozi, Muriithi alionekana kati ya magavana wachapakazi kutoka Ukanda wa Mlima Kenya na kupigiwa mfano na serikali kwa utendaji uliotukuka.

Serikali aliyokuwa akiiongoza Muriithi iliimarisha miundombinu na pia kuunganisha maji katika maeneo kame kwenye kaunti ndogo ya Mukogo, Laikipia Kaskazini.

Alikuwa kati ya magavana ambao waliimarisha mapato ya magatuzi yao, kwa kukusanya ushuru wa shilingi za Kenya zinazofikia bilioni moja kufikia mwishoni mwa mwaka wa kifedha wa 2021/22 mnamo Juni.

# Watu wenye sifa hawapatikani kwa bahati

**Na Askofu Dkt. Stephen Munga**

KATIKA toleo lililopita nilieleza kuwa mtu ni kuwa na sifa za utu. Huyu ni mtu aliyepambwa na vipawa vya asili na vile viitavyo vipawa maalum.

Vipawa hivi ndivyo huonyesha uwezo wa kila mtu kuishi kama yeye binafsi; mvuto na uweleweka wake kwa jamii; na nguvu ya karama zake za utumishi wake kwa jamii na uumbaji kwa jumla.

Kwa hiyo, mtu ni nguvu na uwezo ulioko ndani ya kila mmoja, lakini pia ni jinsi nguvu na uwezo huo unavyoweza kujitokeza kwa namna mtu anavyohusiana na watu wengine (personal and relational).


Uhusiano hapa unachukua dhana pana kuanzia maisha binafsi na wengine kwenye ndoa, familia, shuleni, kazini, michezoni, kwenye uongozi, kwenye kufanya siasa, n.k.

Vilevile nimesema kwamba mtu huyo katika kuishi kwake na kutumia vipawa vyake, anajua kuvitumia na kwa wale wanaguswa na matumizi ya vipawa hivyo. Hapa ndipo hutokeza dhana nyingine ya kuaminika kwa wale anaohusiana nao.

Uzoefu wa upungufu uliyotokea katika maisha ndio umesaidia kuweka sheria ya kuratibisha uwajibikaji - nilitoa mfano wa Torati katika maisha ya Taifa la Israeli.

Katika uhusiano huo kila mtu ana uwezo wa kutambua uwepo wa watu wengine, ukiwemo awezo wa kutambua na kuheshimu haki, uhuru na heshima ya wengine; na wajibu wake kwa wengine na uumbaji wote.

Dhana ya uhusiano na mwingiliano katika kuishi ndio hutupa uelewa wa watu kwamba mtu ni kuthibitika kwa kuwepo wake na utambuzi wa uwepo wa wengine na kukubali hivyo.



*Mwalimu Nyerere, muasisi wa Tanzania*

Hivyo ieleweke kuwa “watu” siyo watu-watu tu. “Watu” lazima wawekewe maelezo (qualified) ili uzito na sababu uwepo wake vionekane. Ieleweke kuwa watu ndio chimbuko la ubora au ubaya wa magurudumu yale mengine mawili – siasa safi na uongozi bora.

Hii ndio sababu kubwa kwamba wajibu mkubwa wa kwanza wa taasisi za jamii ni kufanya maandalizi mazuri ya ‘kuzalisha’ watu bora watakaofanya siasa safi na kuwa viongozi bora.

Hapa taasisi za kijamii ni pamoja na zile zinazojihusisha na uzalishaji, malezi, makuzi, maandalizi, utayarishaji wa watu bora. Kutengeneza watu wazuri ni wajibu wa kwanza wa jamii yeyote yenye maono na malengo chanya juu ya kesho yake.

Watu wenye sifa hizo hawapatikani kwa kubahatisha, bali kwa mipango na malengo ya makusudi. Katika malengo hayo lazima dhamira zitamani kwamba kila kizazi kinachofuata kiwe bora na mahiri kuliko vizazi vilivyotangulia. Pasipo kufanya hivyo, basi ubora wa jamii utaporomoka.



Na Evarist Chahali
evarist@chahali.com

# Tupunguze umaskini kuondoa ugaidi

JUMANNE wiki iliyopita, Wakenya walipiga kura katika uchaguzi mkuu ambapo pamoja na nafasi nyingine zilizokuwa zinawaniwa, ni urais wa taifa hilo la eneo la Afrika Mashariki.

Japo hadi wakati makala haya yanaandikwa, matokeo katika nafasi ya urais hayajatangazwa rasmi, uchaguzi huo umepata sifa lukuki kutoka sehemu mbalimbali duniani.

Sifa hizo zimeelekezwa zaidi katika jinsi uchaguzi huo ulivyoendeshwa kwa uwazi mkubwa. Hata hivyo, kama nilivyotanabaisha kwenye makala katika toleo lililopita la gazeti hili, moja ya changamoto zilizokuwa zikiukabili uchaguzi huo ni tishio la ugaidi kutoka kwa kikundi cha al-Shabaab.

Kwa hiyo, wakati pongezi zinaelekezwa kwa taasisi mbalimbali zilizoweza kufanikisha uchaguzi huo, hususan Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC), mashujaa wasiosikika ni vyombo vya dola nchini humu, hususan Idara ya Usalama wa Taifa ya Kenya (NIS).

Ilikuwa ikifahamika kuwa al-Shabaab wangejaribu kuhujumu uchaguzi huo, na kwa vile zoezi la kupiga kura limeisha salama, ni dhahiri kuwa vyombo vya dola nchini humo vimeweza kuwadhibiti magaidi hao.

Hata hivyo, changamoto ya ugaidi ni endelevu hasa kwa kuzingatia ukweli kwamba wakati vyombo vya dola vinahitaji kila sekunde kuhakikisha magaidi hawafanikiwi katika azma yao ovu, magaidi hao wanahitaji sekunde tu kutimiza uovu wao. Kwa lugha nyingine, wakati vyombo vya dola vinapaswa kuwa macho muda wote, magaidi wanahitaji fursa moja tu.

Mafanikio hayo ya vyombo vya usalama vya Kenya kudhibiti uwezekano wa mashambulizi ya kigaidi kutoka kwa al-Shabaab yamekuja wakati ripoti ya



*Rais Uhuru Kenyatta wa Kenya*

kitaalamu iliyowasilishwa kwa Umoja wa Mataifa wiki iliyopita imeonya kwamba Bara la Afrika linaweza kuwa uhalifa (caliphate) mpya wa kikundi cha kigaidi cha kimataifa cha ISIS.

Jumanne iliyopita, mtaalam wa usalama wa bara la Afrika, Martin Ewi, alilieleza Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kwamba hadi sasa takriban nchi 20 barani humo zinaguswa moja kwa moja na vitendo vya kigaidi vya ISIS.

Alitanabaisha kwamba Bonde la Ziwa Chad – ambalo nchi za Chad, Nigeria, Niger na Cameroon zinapakana – ndilo limekuwa eneo kuu la operesheni za kigaidi za ISIS, huku maeneo katika ukanda wa Sahel yakiwa "hayatawaliki" (kutokana na mashambulizi ya ISIS), na Somalia imeendelea kuwa hatari.

Alieleza kuwa japo jaribio la ISIS kuiyumbisha Uganda limeshindwa, matawi ya kundi hilo nchini Msumbiji na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) yanaendeleza mauaji katika nchi hizo.

Nitoe mwito kwa serikali barani Afrika, ikiwa ni pamoja na Tanzania, kuongeza jitihada za kupunguza umasikini, ambao, japo siyo sababu ya moja kwa moja ya watu kujiunga na ugaidi, inachangia kwa kiasi kikubwa kuwepo kwake.

# Mafuta: Zigo zito kwa Rais Samia

**Na Mwandishi Wetu**

WATUMIAJI wakubwa wa mafuta ya taa, dizeli na petroli nchini Tanzania 'wanaumia' mno kutokana na kupanda bei kwa nishati kila mwezi.

Kupanda kwa bei ya mafuta kunalalamikiwa kila uchao, siyo na wenye viwanda na magari pekee, bali hata wanaotumia nishati hiyo majumbani. Kwa kifupi mafuta kwa sasa hayashikiki – kila mmoja analalamika.

Taarifa za kupanda kwa bei ya mafuta zinazotolewa kila mwezi na Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji Tanzania (Ewura), zinaonyesha kupanda kwa wastani wa Sh.200 kwa kila mwezi – kwa kila lita moja kuanzia Juni, mwaka huu.

Endapo mafuta hayo yataendelea kupanda, hadi kufikia Oktoba, mwaka huu, upo uwezekano mkubwa kwamba nishati hiyo kuuzwa hadi shilingi 4,000 kwa lita moja katika baadhi ya maeneo ya nchi.

Inaelezwa kuwa kupanda bei kwa nishati hiyo muhimu katika uzalishaji wa bidhaa, hakuwaumizi waagizaji wakubwa ama wanunuzi wa jumla peke yao, bali zaidi sana wenye viwanda, mitambo, magari na watumiaji wa nyumbani.

Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa anaeleza kwamba ili kukabiliana na changamoto hiyo, serikali iko katika mchakato wa kupata ufumbuzi wa kupunguza makali hayo ya kupanda kwa bei ya mafuta nchini.

Anasema kupanda kwa bei ya mafuta ni tatizo la dunia nzima na kwamba serikali haipaswi kulaumiwa kwa kadhia hiyo ambayo haijaathiri Tanzania pekee, bali maeneo mengi ya dunia.

Msigwa anabainisha kuwa moja ya mbinu ambazo Tanzania imeanza kutumia ni kutoa ya ruzuku ya shilingi bilioni 100 kwa ajili ya kupunguza bei ya nishati hiyo.

Hata hivyo, hali hali inaonyesha kuwa pamoja na kutolewa kwa ruzuku hiyo kwenye mafuta, bado bei inapanda kila mwezi na kuonekana "msaada" kwa kiwango kidogo.

Mwezi Julai 2022, bei ya petroli ilipanda kwa Sh. 190 kwa kila lita na 179 kwa kila lita ya dizeli, huku mafuta ya taa yakipanda kwa Sh. 323 kwa kila lita katika jiji la Dar es Salaam.

Taarifa iliyotolewa mapema Agosti, mwaka huu na Ewura, inaonyesha kuwa bei ya rejareja ya mafuta katika Jiji la Dar es Salaam ilifikia Sh. 3,410 kwa lita moja ya petroli na Sh. 3,322 kwa dizeli, huku mafuta ya taa yakifika Sh. 3,765.

Inaelezwa kuwa pamoja na bei hizo kuonekana kupanda, bado ni nafuu ikizingatiwa kuwa zina nafuu ya ruzuku kutoka serikalini. Vinginevyo bei zingekuwa juu zaidi.

Msigwa anabainisha kuwa bei za mafuta katika soko la dunia zimeendelea kuongezeka na kusababisha bei za mafuta katika soko la ndani kuongezeka pia, ingawa baadhi ya wachumi wanaeleza kinyume chake.

Mohammed Rahim, mfanyabiashara wa magari ya mizigo jijini Dar es Salaam, anasema kuwa bei ya mafuta katika soko la dunia kwa sasa inapungua, lakini haelewi kwanini Ewura wanaendelea kupanga bei za juu.

"Siwezi kujua sababu, lakini kitu dhahiri ni kwamba bei ya mafuta kwa pipa moja kwenye soko la dunia, inaendelea kupungua katika soko la dunia, lakini hapa kwetu, kila mwezi tunatangaziwa kupanda kwa bei, sasa kuna mkanganyiko hapa," anasema Mohammed.

Anasema sehemu kubwa ya fedha anazotumia katika magari yake ya kusafirisha mizigo mikoani na nje ya nchi, hutumika kununua mafuta na kwamba faida yake imemegwa kwa zaidi ya asilimia 65.

"Mwanzoni kabla ya kuwepo kwa ongezeko la bei ya mafuta, nilikuwa Napata faida, siyo kubwa sana, lakini inayohimili uendeshaji wa biashara, lakini sasa ni maumivu tu, kutokana na kupaa kwa bei ya mafuta, ikiwa hali itakuwa hivi,

# Mafuta: Zigo zito kwa Rais Samia

basi itabidi biashara zisimame kwanza, maana hata wateja hawatakuwepo," anasema kwa masikitiko.

Mhadhiri wa vyuo vikuu, Dkt Lenny Kasoga akizungumzia kadhia hii ya kupanda kwa bei ya mafuta anasema kwamba, serikali inabidi kujipanga zaidi na kuona namna bora ya kuleta nafuu kwa wananchi wake.

Anashauri kwamba ni vyema sasa serikali ikaona umuhimu wa kutoa ruzuku kubwa kwa bei ya mafuta ya petrol kwani ndiyo muhimili wa uzalishaji wa bidhaa.

Dkt. Kasoga anasema Rais Samia Suluhu Hassan, aache kutoa ruzuku kwenye aina nyingine ya mafuta, isipokuwa dizeli pekee ili wenye viwanda na wenye mitambo mikubwa wapate unafuu.

"Kama Rais Samia bado ataendelea kutoa ruzuku ya mafuta, basi iwe kwenye viwanda na mitambo mingine mikubwa ya uzalishaji, inayotumia zaidi mafuta mazito – dizeli, na aachane na petroli, hapo atakuwa amesaidia zaidi," anashauri Dkt. Kasoga.

Anasema kwamba wenye viwanda wakipata unafuu kwenmye dizeli, huenda bei ya bidhaa zinazozalishwa ikapungua na kuleta unafuu kwa wateja wa mwisho.

Mchumi Adolf Mazinge wa Kampuni ya Cosco ya Dar es Salaam, anashangaa kupanda kwa bei ya mafuta kila mwezi kwa maelezo kwamba bei ya nishati hiyo kwenye soko la dunia imeshuka.

Anasema kwamba Ewura inapaswa kuwaeleza wananchi sababu za kupanda kwa bei ya mafuta, licha ya kuwepo unafuu wa bei katika soko la dunia kwa sasa.

"Hivi sasa bei ya mafuta kwa pipa moja katika soko la dunia imeshuka, lakini hapa kwetu kwa miezi minne mfululizo, tunashuhudia kupaa kwa bei ya mafuta, serikali ieleze sababu kuliko, isikae kimya," anashauri.

Anadai kwamba mara ya mwisho bei ya mafuta katika soko la dunia ilipanda Juni 5, 2022 ambapo bei ya pipa moja



la mafuta yasiyosafishwa ilifikia Sh. 285,572.

Mchumi huyo anadai kwamba kutokea mwezi huo, bei ya mafuta kwa pipa moja imeendelea kushuka bei na hadi kufikia mwanzoni mwa mwezi huu- Agosti, bei hiyo imefikia Sh. 237,209.

Pambazuko imeona bei ya mafuta yasiyosafishwa – kwa wiki iliyoishia jana, kufikia Sh. 211,876 katika soko la dunia na kwamba huenda nishati hiyo ikaendelea kushika kuelekea mwishoni mwa mwaka huu.

Sababu zinazoelezwa na serikali kuhusu ongezeko la bei ya mafuta ni vita vya Russia na Ukraine na kudorora kwa uchumi wa dunia katika nusu ya mwaka huu – 2022.

Hata hivyo, uchunguzi wa Pambazuko unaonyesha kwamba kudorora kwa uchumi wa dunia, hakujaathiri sana nguvu ya soko la fedha, hasa ya shilingi ya Tanzania dhidi ya dola ya Marekani; hadi sasa dola moja ni sawa na Sh. 2,310.

Wachumi wanaeleza kwamba shilingi ya Tanzania haijashuka thamani kwa zaidi ya asilimia 0.98 katika kipindi cha miezi minne kuanzia Aprili, 2022.

Kwamba kuporomoka kidogo kwa thamani ya shilingi ya Tanzania, bado hakuwezi kufanya bei ya mafuta kuongezeka kila mwezi kwa kiwango kinakaribia sh. 200.

Taarifa kutoka serikalini zinaeleza kuwa mafuta yanayoingizwa nchini, huanza kutumika baada ya mwezi mmoja na nusu hadi miwili, hivyo kunapotokea ongezeko la bei, huakisi mafuta yaliyoingia nchini kwa kipindi hicho.

# Tutakumbuka Daima...



*Aprili 24, mwaka 1964, Spika wa Bunge la Tanzania, Chifu Adam Sapi Mkwawa (kushoto) alimkaribisha Rais wa Tanganyika, baadaye Tanzania (baada ya Muungano wa Tangayika na Zanzibar), Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, kulia, kuhutubia bunge. Bunge wakati huo lilikuwa likifanya mikutano yake jijini Dar es Salaam. (Picha kutoka Maktaba ya Pambazuko).*

# Ngeli za Nomino




**Na Dkt. Michael Mashauri**

KISWAHILI ni miongoni mwa lugha zinazokua kwa kasi kubwa kila siku duniani. Vyuo vikuu nje ya Afrika, vimeanza kufunza lugha hiyo adhimu. Kutokana na umuhimu wake, Pambazuko limeamua – kila wiki, kuwa njia ya kufundisha Kiswahili bure kwa yeyote anayependa.

Leo mwalimu ataelezea kuhusu majina. Kwamba majina yote katika Kiswahili yamegawanyika katika makundi yanayoitwa ngeli za nomino (noun classes).

Aina ya uainishaji wa makundi hayo inayotumika zaidi kuyagawa ni ile inayozingatia viambishi vya umoja na wingi. Majina yenye viambishi vya umoja na wingi vinavyofanana huunda kundi moja.

Hata hivyo, kuna baadhi ya majina yana tabia tofauti na hii. Pia, kila kundi la nomino huwa na sifa fulani za kisemantiki sanjari na viambishi awali.

Aidha, kila ngeli huwa na viambishi mahsusi vya upatanisho wa kisarufi katika vitenzi na vivumishi.

***(All names in Swahili are divided into groups called noun classes. The kind of classification which considers singular and plural prefixes is mostly used to classify these groups. Names with similar sg/pl prefixes create one group of nouns. However, there are some nouns that behave differently. Moreover, every noun class has certain semantic features that identify it together with sg/pl prefixes. Also, each noun class has specific affixes for agreement in the verbs/adjectives.***

**M/WA noun class**

Ngeli hii hujumuisha majina ya viumbe hai (binadamu, wanyama, ndege na wadudu). Viambishi vyake vya umoja ni **M-, MU-** au **MW-** na wingi ni **WA-**. Ikiwa nomino inaanza na konsonanti huwa **M-,** ikianza na irabu tofauti na /u/ huwa **MW-** na ikianza na irabu /u/ huwa **MU-.**

This noun class comprises all animates (people, animals, birds and insects). Its singular prefixes are **M-, MU-** and **MW-** and plural is **WA-**. If the roots of a noun begins with a consonant it takes **M-**, with a vowel other than /u/ it takes **MW-** and when it begins with /u/ it takes **MU-.** Examples:

| Prefixes | | Class | Root | Examples | | English translation |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Singular | Plural | | | Singular | Plural | |
| m- | wa- | m-/wa | -tu | mtu | watu | Person/persons |
| m- | wa- | | -tanzania | Mtanzania | Watanzania | Tanzanian/Tanzanians |
| mw- | wa- | | -anafunzi | mwanafunzi | wanafunzi | Student/students |
| mu- | wa- | | -uguzi | muuguzi | wauguzi | Nurse/nurses |

• ***Mwandishi wa Darasa la Kiswahili ni Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.***

# Serikali yajipanga kunufaika kwa madini

SEKTA ya madini nchini Tanzania ni sekta muhimu sana kwa maendeleo ya taifa la Tanzania, moja ya vitu muhimu ni ushirikishwaji wa wananchi katika sekta hii kwa ajili ya maendelo ya uchumi wa taifa kutoka uchumi wa chini na kuelekea uchumi wa kati.

Katika kipindi cha miaka kadhaa iliyopita, serikali iliamua kuanza ujenzi wa vituo kadhaa kwa ajili ya shughuli mbalimbali zinazohusiaja na madini, ikiwamo kuuza na kununua madini.

Miongoni mwa vituo vilivyojengwa ni pamoja na kituo cha Musoma, kilichopo mkoani Mara ambacho kimegharimu kiasi cha Sh. 1,211,861,180.00. Ujenzi wa jengo hili unajumuisha ujenzi wa jengo kuu, ujenzi wa banda la kuchakatia madini , kibanda cha klinzi, kazi za nje - ikiwa ni pamoja na ujenzi wa ukuta.

Aidha, katika jengo kuu kutakuwa na ukumbi wa mikutano kwa ajili ya mafunzo mbalimbali na maonesho ya shughuli za madini. Vilevile, kutakuwa na maabara ndogo kwa ajili ya kupima sampuli mbalimbali za madini. Kwa sasa ujenzi wa jengo hili umekamilika

Pia katika mpango huohuo, kuna ujenzi wa mradi wa dhahabu wa Buhemba, mkoani Mara ambapo shughuli zilizotekelezwa ni kukamilika kwa ununuzi wa mtambo wa kuzalisha dhahabu kwa kuchakata mabaki ya dhahabu; kufanya shughuli za awali na uchorongaji katika eneo la mashapo ya mwamba mgumu kwenye mgodi; na kukamilika kwa upembuzi yakinifu katika mabaki ya dhahabu yaliyoachwa kipindi cha nyuma ambapo umebaini kuwapo kwa takribani tani 796,400 za mabaki ya mchanga wa dhahabu yenye wastani wa kilo 852 za dhahabu.

Kadhalika, mradi wa kuendeleza mgodi wa makaa ya mawe wa Kiwira ambao ni mgodi wa makaa ya mawe wa kuzalishauUmeme wa MW 200, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na kuendelea na uchimbaji na kuanza uoshaji wa makaa ya mawe ikiwa ni pamoja na ununuzi wa vifaa vya uchimbaji na mtambo wa kuoshea makaa hayo kwa ajili ya kuyaongezea thamani; kuanza uzalishaji wa nishati mbadala (coal briquette) kwa ajili ya matumizi ya nyumbani; na uzalishaji wa tani laki 1.6 za makaa ya mawe.

Aidha, serikali ilikamilisha ujenzi wa ukuta wenye mzingo wa km 24.5 kuzunguka migodi ya Tanzanite Mirerani na uwekaji wa mfumo wa ulinzi wa kidigitali ambao umewezesha kupunguza utoroshwaji wa madini.

***•Makala haya yamepatikana kutoka wavuti rasmi ya serikali ya Tanzania; www.miradi.uwezeshaji.go.tz***



# Padre Didace: kukata tamaa ni dhambi

**Na Deusdedith Kahangwa**

"MIAKA michache baada ya kupata upadre nilipata ajali mbaya ya gari. Kwa sababu hiyo, niliumia na kulemaa uti wa mgongo. Tangu wakati huo, sijaweza kusimama wala kutembea tena kwa miguu yangu. Na mpaka sasa najongea kwa kutumia kiti cha umeme ninachokiendesha mwenyewe."

Haya ni maneno ya Padre David Bimenyarugaba Didace (pichani). Kituo chake cha kazi kiko katika Jimbo la Rulenge-Ngara. Alizaliwa katika Wilaya ya Ngara, mkoani Kagera.

Katika miaka ya 1990, alimaliza elimu ya kidato cha nne katika Seminari Ndogo huko mkoani Kagera. Baadaye alijiunga na masomo ya falsafa kwenye Seminari Kuu, Mkoani Kagera. Pia, akiwa Seminari Kuu iliyoko mkoani Tabora, alisoma tHeolojia. Hatimaye alipata upadre.

Baadaye alijiendeleza hadi Chuo Kikuu alikopata Shahada ya kwanza ya elimu dunia katika utawala na uongozi wa taasisi za kibinadamu.

Mara tu baada ya kupata shahada hii, katika miaka ya 2000, alipatwa na ajali mbaya ya gari. Katika ajali hiyo, aliumia uti wa mgongo. Lakini, anasema kuwa, kuumia na kulemaa uti wa mgongo siyo kikwazo kwa utumishi wake kama padre na mtaalamu mshauri wa masuala ya kijamii.

"Namshukuru Mungu sana kwa sababu bado ninayo nafasi ya kutumika kama padre wa kawaida. Na kama mtu mwenye taaluma zaidi ya masomo ya kipadre, naweza kufanya ushauri na unasihi kwa wananchi ndani na nje ya Kanisa. Najiona mwenye manufaa kwa jamii," anasisitiza Padre Didace.

Pamoja na kwamba yeye anaishi akiwa mlemavu, bado anaishi kwa furaha, na anafanya kazi za kitumishi kama kawaida. Anaendelea kuitumikia jamii kwa karama



alizopewa na Mungu na kwamba anashukuru watu wanaoamini katika uwezo wake wa kutenda na kusaidia pale anapoweza. Anashukuru Kanisa na jamii inayoendelea kumthamini.

Padre huyo anaeleza kuwa anaendelea kuishi kwa matumani, na kumwomba Mungu daima, anasema; "pamoja na ulemavu huu, bado mimi ni sura na mfano wa Mungu, na Mungu wetu ni Mwema siku zote.

Anasema ulemavu siyo mwisho wa utumishi wala maisha na watu wenye hali kama yake hawapaswi kukata tamaa, kwani ni dhambi.

# PICHA KUBWA



*Jakaya Kikwete, Rais (mstaafu) wa Tanzania, ambaye alikuwa kiongozi wa wasimamizi wa uchaguzi mkuu Kenya - kutoka Jumuia ya Afrika Mashariki (EAC) akiwa na mgombea urais katika uchaguzi huo kwa tiketi ya chama cha Roots, Prof. George Wajackoyah Alhamisi iliyopita Jijini Nairobi. Uchaguzi huo ulifanyika Jumanne iliyopita – Agosti 9, 2022. (Picha kutoka ukurasa wa Twitter wa mgombea huyo).*

*GAZETI hili huandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi na Habari Tanzania (Tampa). Pambazuko limesajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448.*

TAMPA
TANZANIA MEDIA PRACTITIONERS ASSOCIATION